

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA SABA

06 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA SABA – TAREHE 06 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA
BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. •

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA
MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

139. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Daraja katika Mto Mzizima ili Barabara ya Kigwe - Chipanga iweze kupitika Mwaka mzima.

140. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Serikali isije na mkakati katika Bajeti ya 2022/23 wa kujenga Shule za Msingi kwenye Vitongoji vyenye Watoto zaidi ya 200.

141. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Watumishi Manispaa ya Mpanda katika maeneo ya Afya, Elimu na Maendeleo ya Jamii.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

142. MHESHIMIWA ESTER EDWIN MALEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, ni lini Serikali itaongeza Wataalam wa Saikolojia ili kutoa huduma za ushauri wa afya ya akili na namna ya kuondokana na msongo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

143. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Bodi za *Parole* za Mikoa na Kitaifa zina vikao vingapi kwa Mwaka na wafungwa wangapi wamepata msamaha kwa Mwaka 2020/2021.

WIZARA YA MAJI:

144. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA KITANDULA (MKINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini ujenzi wa Mradi wa Maji Mkinga kutoka Mto Zigi au Kinyatu utaanza kutekelezwa.

145. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):

● Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- ●

Je, ni lini Serikali itajenga upya Bwawa la Kasamwa na kutenganisha mwingiliano wa binadamu na mifugo.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

146. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itafupisha muda wa miaka 7 kwa Elimu ya Msingi na 6 ya Sekondari ili kupunguza muda kwa Wanafunzi wenye uwezo mkubwa.

WIZARA YA KILIMO:

147. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mkoa wa Rukwa unalima zao la Maharage lenye uhitaji mkubwa zaidi Duniani.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

148. MHESHIMIWA EMMANUEL MAGENI KASALALI (SUMVE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Km 73 kutoka Fulo - Nyambiti - Malya itanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

149. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini ujenzi wa Madarasa katika Kampasi ya Chuo cha Uvuvi Kibirizi utanza.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA
BIASHARA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**06 MEI, 2022
DODOMA**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**